

HOTUBA YA MKE WA RAIS WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA MHE. MAMA SALMA
KIKWETE KATIKA UZINDUZI WA MAFUNZO YA UUGUZI
KATIKA TAASISI YA A3.

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Leonidas Gama

Mwenyekiti wa K.S.I. (Koja Shia Ithnaasheri) Jamaat, Dar es Salaam, Ndugu, Shiraz Walji,

Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu , Dr. Jaffer Dharsee,

Mjumbe wa Bodi ya Elimu, Bibi Fatim Somji,

Ndugu Mustafa Sabodo,

Wamiliki na Kamati ya Menejimenti na Ofisi nyingine za K.S.I Jamaat Dar es salaam,

Uongozi na Wakufunzi wa Taasisi ya masomo ya kitaalamu ya A3

Wakuu na Makamu wa Shule za Al muntazir,

Wawakilishi kutoka Wizara mbalimbali,

Wapendwa Wageni Waalikwa,

Wapendwa wanafunzi,

Asalaam Alaikum,

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo. Najisikia furaha kubwa sana kuwa nanyi katika mkusanyiko huu, kwa ajili ya shughuli hii muhimu sana ya uzinduzi rasmi wa mafunzo ya uuguzi katika taasisi hii ya masomo ya kitaalamu ya A3.

Wapendwa Wananchi,

Kitu pekee ambacho kinatofautisha nchi zilizoendela na zinazoendelea sio utajiri na mali bali ni elimu. Hii ni kwasababu utajiri na mali havijileti vyenyewe kwa mtu na wala havirithishwi bali ni matokeo ya mambo mengine ikiwemo ELIMU. Hivyo ni kiwango cha elimu na ujuzi ndicho kinachotofautisha nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea. Kwa kadri kiwango cha elimu na ujuzi au maarifa kinapokuwa juu katika nchi, ndipo na kiwango cha mali na utajiri nacho kinavyozidi kupanda katika nchi hiyo.

Kutokana na sababu hii basi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira ya dhati kabisa imeamua kuwekeza sana katika sekta ya elimu. Kuwekeza huku ni katika suala la rasimali fedha na rasilimali watu. Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.

Jakaya Mrisho Kikwete hata katika hotuba yake ya kuzindua Bunge la kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alisema wazi kuwa kipaumbele katika bajeti ya nchi yetu itakuwa ni katika suala la elimu. Na hata sisi leo nimashahidi kwani katika awamu hii kuna shule nyingi sana za Sekondari za kata zimejengwa, na hata chuo kikuu cha Dodoma nacho pia kimeshaanza kutoa wahitimu wake ambapo miongoni mwao ni walimu. Haya yote ni katika kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata elimu. Mie naamini kama ambavyo Taasisi ya A3 na nyote hapa mlivyodhihirisha, kwa kadri kiwango cha elimu cha Tanzania kinapokuwa juu, ndivyo maendeleo na utajiri wa nchi yetu nao utakavyoongezeka.

Katika juhudi hii ya kuinua kiwango cha elimu na ujuzi wa nchi yetu, ndipo tunapotambua nafasi ya mwanamke katika jamii.

Wapendwa Wananchi,

Charles D. Mclver alisema ***“Unapomuelimisha mwanaume, umemuelimisha mtu mmoja, ukimuelimisha mwanamke umeelimisha familia”***. Hata hivyo mimi imani yangu ni zaidi ya hapo, kwani naamini ukimuelimisha

mwanamke ni zaidi ya kuelimisha familia nzima, bali unaelimisha jamii yake.

Aidha naungana na ule msemu aliosema Makamu wa Rais wa Afrika ya Kusini, Mhe. Phumzile Mlambo Ngcuka katika mkutano wa nne wa mwaka wa Wabunge wanawake jijini Capetown, Afrika Kusini, tarehe 28 mwezi wa Nane, 2007, yeye alisema “ *Ukimuelimisha mwanamke umeelimisha Taifa*”.

Kwani unapomuelimisha mwanamke unakuwa umemuwezesha, umempa uhuru, umempa hadhi na umempa nafasi katika jamii. Na hii ndiyo sababu iliyonifanya nianzishe taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA). Nilianzisha WAMA kutokana na shauku na hisia zangu katika kumuendeleza mwanamke wa Kitanzania. Nataka kuona nchi yetu inaendelea, na kwasababu hii, wanawake wa nchi yetu wanahitaji kuelimishwa na kuwezesha.

Ndugu Wananchi,

Nimeguswa sana na mtazamo wa Taasisi hii ya masomo ya kitaalamu ya A3 kuhusu WAMA. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa na asanteni sana kwa kuamua

kumuelimisha mwanamke kupitia WAMA. Tutatumia vizuri fursa mlizotupatia kwa kuwatambua walengwa wanaostahili. Naamini, ni kwa ushirikiano na watu wenye Moyo wa kujitolea kama nyinyi, ambapo tunaweza kubadili maisha ya vijana wetu wenye mahitaji.

Inatia moyo kushuhudia ongezeko la taasisi za Elimu ya juu kama hii taasisi ya masomo ya kitaalamu ya A3. Nafarijika zaidi pia kujua ni taasisi dada ya shule za Al Muntazir. Nimezijua shule za Al Muntazir kwa muda mrefu sasa, Al Muntazir inafahamika sana katika upande wa elimu katika nchi yetu. Hata watoto wangu wanasoma katika shule ya Msingi ya Wavulana ya Al Muntazir.

Napenda kuipongeza K.S.I. Jamaat, Bodi ya Elimu na Bodi kuu ya Elimu kwa kuingia katika hatua hii ya kitaalamu ya elimu ya juu. Sasa napenda mfikirie kuchukua hatua nyingine zaidi ya kuanzisha Chuo kikuu.

Mwisho kabisa nashukuru ungozi wa Taasisi ya masomo ya kitaalamu ya A3 kwa kunialika kuzindua rasmi mpango wa mafunzo ya uuguzi. Asanteni sana. Nawashukuru vijana walioimba kwa ustadi na uzalendo mkubwa.

Nawatakia kila la kheri wanafunzi wote katika masomo yenu.

Kwa kusema hivyo basi, naomba nitamke kwenu kwamba
mpango wa mafunzo ya uuguzi umezinduliwa rasmi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA!